

Je, Ikiwa Mtoto Wangu Hastahiki Elimu Maalum?

Timu ya elimu maalum inaweza kuamua kuwa mtoto wako hastahiki kupokea huduma za elimu maalum. Ikiwa hukubali na uamuzi huo, una machaguo kadhaa:

Unaweza kuomba tathmini nyingine.

Ikiwa itaidhinishwa, tathmini itafanywa na mtu ambaye hafanyi kazi kwenye wilaya ya shule. **Tathmini zote zitalipwa na wilaya ya shule.**



Nchini Marekani, watoto wote wana haki ya elimu ya umma ya bila malipo na inayofaa.



Unaweza kuwasilisha malalamishi au kuomba mapatano.

Unaweza kujifunza kuhusu machaguo haya katika **Notisi ya Kinga za Taratibu. Lazima** shule yako ikupe waraka huu kwa lugha unayopendelea na kwa njia unayoelewa.

Ikiwa mtoto wako hastahiki kupokea IEP, unaweza kuomba **Mpango wa 504**. Ikiwa mtoto wako anastahiki, mpango huu unatoa huduma na hisani za kushiriki shuleni.